# TAARIFA KWA UMMA

**Septemba 14, 2025**

Katika siku za hivi karibuni kumeibuka vitendo viovu vinavyofanywa na baadhi ya watu wenye nia ovu kwa kusambaza picha mnato na picha mjongeo (video) za matukio ya zamani. Maudhui ya picha na video hizi yanalenga kuleta taharuki, kuogofya na kutishia amani ya wananchi, jambo ambalo ni hatari kwa usalama na mshikamano wa taifa letu.

Baadhi ya picha hizo zinaonesha maandamano, matukio ya uhalifu, watu walioumia au waliopoteza maisha, na zinatolewa katika muktadha wa kupotosha au kuchochea hisia hasi miongoni mwa wananchi. Vitendo hivi ni kinyume na Kifungu cha 54 cha Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229 (Toleo la 2023) Kifungu cha 16 cha Sheria ya Makosa ya Mtandao, Sura ya 443 (Toleo la 2023) na Aya ya 10 ya Jedwali la Kanuni za Maudhui Mtandaoni, chini ya Tangazo la Serikali Na. 538 lililochapishwa tarehe 17 Julai 2020, kama lilivyofanyiwa marekebisho.

Wananchi wanaaswa kujiepusha kusambaza au kushabikia maudhui hayo kupitia mitandao ya kijamii au njia nyingine yoyote ya mawasiliano, kwa kuwa kufanya hivyo ni kushiriki katika uhalifu wa mtandaoni. Usalama wa nchi ni jukumu la kila mmoja wetu. Tushirikiane kulinda amani na utulivu wa Taifa letu kwa kutumia mitandao ya kijamii kwa njia chanya, yenye kujenga na kuimarisha mshikamano wa kitaifa. Serikali inatarajia ushirikiano kutoka kwa wananchi wote katika kuhakikisha maudhui ya aina hii yanakomeshwa mara moja.

Aidha, Serikali kupitia vyombo vyake vya usalama tayari imeanza kuchukua hatua, ikiwa ni pamoja na kuwatambua na kuwafuatilia wale wote wanaojihusisha na vitendo hivyo. Hatua za kisheria zitachukuliwa bila kujali hadhi au nafasi ya mtu yeyote atakayebainika kuhusika.

Gerson Msigwa
Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Utamaduni,Sanaa na Michezo
na Msemaji Mkuu wa Serikali